KISWAHILI: KARATASI YA KWANZA: LUGHA

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu swali la 1 hadi la 5.

Maadili ya kitaifa ni tabia njema na mwenendo unaotegemewa kutoka kwa raia wa nchi fulani. Hapa nchini, maadili ya kitaifa yanahusisha mambo kama vile uzalendo, uadilifu, uwajibikaji, haki na mashikamano. Mwanafunzi mtiifu anapaswa kuonyesha maadili haya shuleni kuwa mwaminifu, kuheshimu walimu na wenzake na kushiriki katika shughuli za shule kwa bidii.

Maadili haya hutufundisha kupenda nchi yetu na kuchangia maendeleo yake. Pia husaidia kuimarisha umoja na amani miongoni mwa wananchi. Tunapofuata maadili ya kitaifa, tunakuwa raia bora wenye mchango chanya katika jamii.

1. Maadili ya kitaifa ni nini?

A. Sheria za nchi

B. Lugha ya taifa

C. Rangi ya bendera

D. Tabia njema na mwenendo unaotarajiwa

2. Ni lipi kati ya haya si maadili ya kitaifa?

A. Uadilifu

B. Uwajibikaji

C. Uzembe

D. Haki

3. Mwanafunzi anayekataa kushiriki katika shughuli za kijamii anakiuka maadili yapi?

A. Mshikamano na uwajibikaji

B. Utengano na utangamano

C. Uzalendo na utengano

D. Ukaidi na utiifu

4. Kulingana na kifungu, kwa nini ni muhimu kufuata maadili ya kitaifa?

A. Ili tusiadhibiwe na walimu

B. Ili tuonekane kuwa wasomi

C. Ili kuimarisha umoja na maendeleo

D. Ili kufurahia utengano

5. Kwa mujibu wa kifungu, jukumu la kukuza maadili ya kitaifa linaanzia wapi?

A. Serikalini pekee

B. Mashinani na vijijini

C. Kwa wanafunzi na jamii kwa ujumla

D. Kwa mashirika ya misaada

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu swali la 6 hadi la 12